## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2015 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ifuatayo: 2012, 2013 na 2014.

***Jedwali 9: Matokeo ya KCPE Kiswahili ya 2012 hadi 2015***

| | **2012** | | **2013** | | **2014** | | **2015** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| **Alama ya wastani** | 23.37 | 21.99 | 22.89 | 20.98 | 22.52 | 23.20 | 22.34 | 21.75 |
| **Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi** | 24 | 20 | 23 | 20 | 22 | 24 | 21 | 20 |
| **Alama ya juu iliyotuzwa** | 48 | 39 | 47 | 40 | 47 | 40 | 49 | 39 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba:

**Katika lugha**:

a) Alama ya wastani yaelekea kubakia katika kiwango kilekile; **22.34**, ikilinganishwa na **22.52** mwaka wa 2014.

b) Alama ya juu iliyoweza kutuzwa mwaka wa 2015 ni **49** tofauti na **47** ya mwaka wa 2014.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **21** tofauti na **24** ya 2014.

d) Alama wastani haijafikia kiwango kinachokubalika (25/50).

**Katika Insha:**

a) Alama ya wastani ilishuka kutoka **23.20** mwaka 2014 hadi **21.75** mwaka 2015.


b) Alama ya juu zaidi iliyoweza kutuzwa mwaka 2015 ni **39** tofauti na **40** ya mwaka 2014.

c) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi ni **20** tofauti na **24** ya mwaka 2014.

d) Alama wastani inaelekea kufikia kiwango kinachokubaliwa (**20/40**) japo imepita kiwango hiki kiasi.

Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.


**Fig. 3**




## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

### 4.1.1 Uchanganuzi wa maswali maalum

Mchoro ufuatao unaonyesha asilimia ya watahiniwa ambao walipata jibu sahihi katika kila swali:




### 4.1.2 Uchanganuzi wa maswali yaliyowatatiza watahiniwa

Katika mwaka wa 2015, yapo maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa. Watahiniwa waliopata majibu sahihi kwa maswali haya walikuwa chini ya asilimia thelathini (30%). Maswali yafuatayo ndiyo yanayochukuliwa kuwa yaliwatatiza wanafunzi zaidi: 23, 26, 33, 35 na 45.

*Jedwali 10: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa*

| Maswali | 23 | 26 | 33 | 35 | 45 |
|---|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sahihi | 18.98 | 18.11 | 14.03 | 17.24 | 18.52 |
| Asilimia ya wastani ya mswali yale mengine | 25.70 | 23.89 | 25.03 | 24.45 | 22.65 |

### 4.1.3.1 Ruwaza za majibu

**Swali la 23**

Chagua jibu lenye maelezo sahihi.

A. Kefule! Ni tamko linaloonyesha kuudhika.
B. Hewala! Hutumiwa baada yan kuupata ushindi fulani.
C. Simile! ni tamko linalotolewa baada ya kumruhusu mtu kupita.
D. Makiwa! Hutumiwa ili kumpa pole mtu aliyepoteza bidhaa zake.

**Matokeo ya swali la 23**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 18.98 | 33.02 | 23.18 | 23.17 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 25.70 | 22.83 | 20.94 | 20.43 |

Swali hili lilitahini matumizi mwafaka ya vihisihi.Yaelekea kwamba idadi kubwa ya watahiniwa iliteua **Hewalla**, kihisishi kinachoonyesha kukubaliana na jambo wala si ushindi.

**Swali la 26**

Chagua jibu lenye maelezo sahihi.

A. Kufisha ni kuviweka vitu hadi viharibike ilhali kuficha ni kuviondoa vitu mahali vinapoonekana.
B. Kisasi ni tendo la kumlipizia mtu kosa alilotenda, na kizazi ni watu wanaoishi katika jamii moja.
C. Zabuni ni zawadi anayopata mtu mashindanoni, na sabuni ni madini yanayotumiwa kusafisha nguo.
D. Kudanda ni kuruka ili kukishika kitu ilhali dada ni ndugu wa kike.

**Matokeo ya swali la 26**

| Majibu | A | B | C | D* |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 10.77 | 42.11 | 27.36 | 18.11 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 21.21 | 23.06 | 20.75 | 23.89 |

Swali hili lilitahini vitate.Yaelekea kwamba watahiniwa wengi waliteua jibu **B,** licha ya kwamba maana

ya kizazi si sahihi.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Je, umewahi kutafakari kuhusu namna wanafunzi wengi, ukiwemo miongoni mwao, wanavyosafiri kwenda shuleni? Yumkini jibu lako kwa swali hili litadhihirisha kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi hutembea kwenda shuleni, wengine hutumia baiskeli, magari ya umma na ya kibinafsi, pikipiki na garimoshi. Bila shaka aina ya usafiri hutofautiana kulingana na uwezo wa kiuchumi na umbali baina ya nyumbani kwa mwanafunzi na shule yake.

Kila aina ya usafiri ina changamoto maalum. Mathalani ikiwa umezungumza na wenzako ambao hutembea kwenda shuleni, haikosi wamekuelezea dhiki wanazokumbana nazo. Licha ya safari za aina hii kuwachosha wanafunzi, ni wazi kuwa wanafunzi wengine hata hukosa masomo kwa sababu ya kutopitika kwa njia wakati wa mvua nyingi. Pengine hata wewe umewahi kujipata katika njia panda baada ya daraja unalovukia kusombwa na maji ya mto uliofurika. Isitoshe, watembeao huweza kuathirika kiafya wakati wa kipupwe. Baridi huweza kuwasababishia pumu au hata kichomi. Wengine huwa katika hatari ya kuteleza kwenye njia zenye matope na kuvunjika viungo vya mwili. Hawa pia wamo katika hatari zaidi ya kutekwa nyara na hata kunyanyaswa kimapenzi.

Wanafunzi wengine **huwahusudu** wale ambao husafiri shuleni, ama kwa gari la shule, au la kibinafsi. Wakiulizwa kuhusu kiini cha husuda hii, wanasema kwamba wenzao hawa hawachoki kwani magari haya yanawachukua kutoka malangoni mwa nyumba zao. Hata hivyo, ukichunguza vyema utapata kwamba hata hawa wana matatizo sugu. Kwa vile magari ya shule huwabeba wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali, magari haya hayana budi kuanza safari mapema. Hili huwalazimu wanafunzi nao kuamka alfajiri na mapema ili kuyawahi magari haya. Matokeo ni kwamba wanafunzi wengi hawadiriki kulala usingizi wa kutosha. Kuna wale ambao hulala saa nne usiku baada ya kukamilisha kazi za darasani, kisha wanaraushwa saa kumi ili kujitayarishia basi la saa kumi na moja. Wanafunzi wa aina hii hukumbwa na uchovu, na bila shaka husinzia darasani.

Isitoshe, wanafunzi wanaotumia usafiri wa umma hulalamikia msongamano wa magari ambao unawafanya kukawia njiani, na hata kupewa adhabu kwa kuchelewa kufika shuleni. Wengine hata hukataliwa na magari ya abiria, eti wanalipa fedha kidogo, na kuwasababishia wenye magari hasara. Wanafunzi hawa huaibika na kulazimika kutembea hadi shuleni. Hali kadhalika, magari ya umma humpa mwanafunzi mazingira ya kujifunzia tabia; nzuri na mbaya. Pamoja na wanafunzi hawa kupata fursa ya kutangamana na wenzao kutoka shule nyingine, wao pia huweza kuathiriwa vibaya na hulka za wasafari wengine. Kuna wale ambao huiga lugha, mitindo ya mavazi, namna ya kutembea, na hata mienendo mingine ya madereva na utingo. Wengine huishia kuwa waraibu sugu wa vileo kutokana na vielelezo wanavyopata kwenye magari haya. Muziki, picha za video, na mazungumzo kupitia vyombo vya habari vilivyo kwenye magari haya huchangia kuzorotesha tabia ya wanafunzi. Hii ni kwa sababu baadhi ya masuala yanayozungumziwa ni ya aibu na hayapaswi kusikilizwa na watu wa umri mbichi.

Ni dhahiri kwamba kila aina ya usafiri ina athari zake. Hata hivyo, Baniani mbaya kiatu chake dawa. Usafiri unahitajika katika kufanikisha masomo ya wanafunzi, na katika uchukuzi wa bidhaa na vifaa mbalimbali ambavyo wanahitaji shuleni. Ni jukumu la kila mwanajamii kuhakikisha kwamba mikakati ifaayo imewekwa ili kukinga dhidi ya madhara yanayoandamana na kila aina ya usafiri. Wanafunzi nao wakae ange kutambua watu ambao huenda wakawatosa katika maovu. Wachuje ya kuiga na ya kukataa.

**Swali la 33**

Chagua madhara ya aina ya usafiri unaozungumziwa katika aya ya **pili**.

A. mvua nyingi, kutatizika kimawazo

B. kupatwa na ajali, kuchukuliwa kwa nguvu

C. kuharibika kwa daraja, majira ya baridi

D. ulemavu mwilini, kuingiliana na mazingira yasiyovutia.

**Matokeo ya swali la 33**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 19.13 | 14.03 | 53.37 | 11.89 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 19.12 | 25.01 | 23.02 | 21.57 |

Hili ni swali la kiuchanganuzi. Mtahiniwa alihitajika kutumia ujuzi wa yaliyomo katika taarifa kuteua jibu sahihi.Watahiniwa wengi waliteua jibu **C**, pengine kwa kuwa hawajasoma viteuliwa vyema, wakang'amua kwamba majira ya baridi si madhara ya usafiri.

**Swali la 35**
Ni jibu lipi sahihi kulingana na aya ya **tatu**?
A. Kutumia gari moja kusafiria humnyima mwanafunzi mapumziko yafaayo.
B. Magari yakianza safari shuleni mapema huwafanya wanafunzi kumaliza kazi mapema.
C. Wanafunzi wakichoka hushindwa kuona umuhimu wa masomo darasani.
D. Kupitia sehemu mbalimbali za gari humfanya mwanafunzi kuraushwa

**Matokeo ya swali la 35**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili** | 17.24 | 15.27 | 25.11 | 40.77 |
| **Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine** | 24.45 | 18.84 | 21.54 | 23.32 |

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kutumia kifungu kujibu. Hata hivyo inaelekea kwamba watahiniwa waliongozwa na tajiriba yao ya kuraushwa kwenda shuleni, wakateua jibu **D.**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Simba na fisi walikuwa marafiki wa kufa na kuzikana. Urafiki wao ulishinda hata uhusiano wa ndugu wa toka nitoke. Ulikuwa ule uhusiano wa, mmoja anapojikwaa dole, anayeuhisi uchungu hasa ni huyo rafikiye. Wenzao porini hawakuisha kuusifu urafiki huu. Hakika hata waliwahimiza watoto wao kuiga mfano wa simba na fisi. Kilichowavutia wanyama zaidi ni hulka ya simba na fisi kuchuma pamoja na kuzikimu familia zao pamoja.

Hali iliendelea hivyo hadi wakati simba na fisi walipojifungua vitinda mimba wao. Uzazi huu ulisababisha mabadiliko makubwa katika maisha yao. Licha ya uzee uliokuwa umebisha hodi, simba na fisi walikuwa na vinywa zaidi vya kulisha. Kadhalika, vitoto hivi vikembe vilihitaji uangalizi zaidi, havingeweza kuachiwa ndugu zao. Hali hii iliwafanya wasiweze kuandamana usasini. Waliafikiana kupishana zamu katika majukumu yao. Wakati ambapo simba angeenda kuwinda, fisi angebaki nyumbani akiwatunza watoto. Zipo baadhi ya nyakati, japo kwa nadra mno, fisi alipojitolea kwenda kuwinda. Jambo lililomtia simba wahaka ni kwamba kila fisi alipobakia nyumbani, chakula walichokuwa wamekihifadhi kwa matumizi ya baadaye kiliota mbawa.

Fisi alipoulizwa hakukosa kauli ya kujitetea. "Mambo yamekuwa magumu siku hizi. Ulezi una changamoto zake. Kumbuka pia tuna waivu. Kozi amekuja hapa na kutaka kuwanyakua watoto wetu. Ilibidi nipambane kwa jino na ukucha kuwaokoa. Katika hali hii nilisahau kuwa ghala lilikuwa wazi. Hata kitali kilipokwisha, nilitahamaki kuwa ghala lilikuwa tupu, ikawa ni yale ya mwangaza mbili...," akasema fisi. Lile ambalo simba hakujua ni kwamba fisi alikuwa akikiiba chakula kujinufaisha yeye na wazazi wake.

**Tabia hii ya fisi iligeuka kuwa ngozi ya mwili**. Simba naye alizidi kumshuku fisi. Hata hivyo, alipoendelea kuuliza kuhusu muujiza wa kutoweka kwa chakula, fisi alimlaghai kwamba kwa kweli chakula kilikuwa kikichukuliwa na simba jike mwingine aliyekuwa akiishi ziwani. Hili lilimchemsha simba roho, akakata shauri kwenda moja kwa moja kukabiliana na hasidi huyo. Simba alisimama ukingoni mwa ziwa huku akiyatazama maji yaliyotulia kana kwamba yanamwogopa. Mbele yake, ndani ya maji, alimwona simba jike mwenzake aliyefanana naye kama shilingi kwa ya pili.

"**Kumbe ni kweli kuwa dada yangu huyu hutuendea kinyume?** Kumbe huyu ndiye anayetaka **kuutia ufa** udugu baina yangu na fisi?" simba alijiuliza.

Simba hakujua vipi, lakini alijipata ndani ya ziwa; hasira imemtuma kupambana na simba jike mwenzake. Alitwaa mafumba yake kumchanachana huyo simba, lakini lo! Alijipata anakipiga kivuli chake pambaja majini. Haukupita muda mrefu kabla ya simba kuhisi mng'ato mkali kwenye mguu wake.

Alipotazama alimwona mamba mkubwa ajabu anaendelea kung'wafua minofu ya nyama kutoka pajani mwake. Alitaka kutoa ukemi lakini akajiasa. "Simba haonyeshi maumivu hata mbele ya matatizo makubwa. Huku kutakuwa kujidhalilisha," simba alijisemea. Baadaye alimrukia mamba kwa hamasa kuu, moto wa mapigano ukawaka. Mapambano yalipokatika, wawili hawa walikuwa wamehasirika si haba. Simba alikuwa amedhoofika mguu, naye mamba akabaki na kigutu cha mkia.

Simba alifika nyumbani akiwa hoi kwa maumivu, majonzi na kukatika tamaa. Fisi alipomtazama, michirizi ya machozi ya mamba **ilimtiririka kama maji bombani**. Alimwendea simba na kutaka kumkumbatia. Hata hivyo, mtazamo wa macho ya simba ulimwonya fisi dhidi ya tendo hili na kumfahamisha fisi kuwa urafiki wao wa miaka na mikaka umefikia ukingoni.

**Swali la 45**

Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?

A. Malezi ya fisi na simba yamehitaji hali isiyo na vikwazo vya maadui.
B. Utetezi wa fisi umefanya simba kutojua manufaa ya wazazi wa fisi.
C. Simba na fisi wamebuni njia ifaayo ya kuyaboresha maisha yao.
D. Kutoshughulikia jambo pamoja kumefanya familia ya fisi na samba kutojitosheleza kwa chakula.

**Matokeo ya swali la 45**

| Majibu | A | B | C* | D |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 18.77 | 18.52 | 18.52 | 42.34 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 22.06 | 21.70 | 22.65 | 22.68 |

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuteua jibu sahihi kulingana na taarifa.
Watahiniwa wengi ,kwa kukosa kuzingatia maana zilizofumbatwa na viteuliwa, waliteua jibu, **D**.

### 4.1.3.2 Hitimisho

Kwa jumla uchanganuzi wa mtihani wa mwaka 2015 umebainisha kwamba utendaji wa wanafunzi katika maswali ya ufahamu unaendelea kuimarika. Asilimia kubwa haikutatizika na maswali ya ufahamu kama ambavyo ilikuwa kawaida katika mitihani ya miaka ya awali. Hata hivyo, bado pana haja ya wanafunzi kufunzwa mikakati bora ya kukabiliana na maswali ya ufahamu.

Kadhalika, imebainika kwamba watahiniwa bado wanafanya vyema zaidi katika ufahamu wa kibunilizi ikilinganishwa na utendaji katika ufahamu wa kimaelezo. Ni muhimu walimu kuwaongoza wanafunzi zaidi katika kujibu maswali ya aina zote mbili za ufahamu. Pia, wanafunzi wanastahili kuhimizwa kusoma kwa mapana ili kukuza stadi za kukabiliana na maswali ya ufahamu wa kuandika.